# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE MKUTANO WA WAKUU WA NCHI ZA AFRIKA KUHUSU RASILIMALI WATU TAREHE 26 JULAI, 2023 JNICC – DAR ES SALAAM

- *Waheshimiwa Wakuu wa Nchi na Wawakilishi wa Wakuu wa Nchi;*

- *Waheshimiwa Makamu wa Marais mliopo;*

- *Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;*

- *Waheshimiwa Mawaziri Wakuu mliopo;*

- *Mheshimiwa Mussa Faki, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika;*

- ***Wakuu wa Misafara;***

- ***Waheshimiwa Mawaziri;***

- ***Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia;- Victoria Kwakwa; …….. na Ujumbe wote wa Benki ya Dunia.***

- ***Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa;***

- ***Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;***

- ***Wawakilishi wa Sekta Binafsi pamoja na Wanataaluma mliopo;***

- ***Wageni Waalikwa wote;***

- ***Mabibi na Mabwana:***

Habari za Asubuhi!

Ninayo furaha kubwa kuwakaribisha nyote nchini Tanzania, hususan hapa Jijini Dar es Salaam, bandari ya salama. Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia fursa hii adhimu ya kukutana hapa ili tuweze kujadiliana na kufikia maazimio kuhusu mada hii muhimu na nyeti kwa maendeleo na mustakabali wa Bara letu la Afrika - Maendeleo ya Rasilimali Watu.

Tulipokea kwa heshima na fahari kubwa fursa ya kuwa mwenyeji wa Mkutano huu muhimu na adhimu. Na kwa kipekee kabisa, nitambue na kupongeza kazi kubwa iliyofanywa na Serikali kupitia Wizara zetu za Fedha na

Mambo ya Nje pamoja na Benki ya Dunia katika kufanikisha shughuli hii. Hakika, mmeutendea haki mkutano huu kwa maandalizi mazuri.

Natambua tuna wageni wengi waliosafiri masafa marefu kujiunga nasi leo na nitumie fursa hii kuwapa pole kwa machovu ya safari na kuwakaribisha Tanzania. Natumai mmepokelewa vyema na mmekirimiwa kwa mila na desturi zetu za Kitanzania. Karibuni sana.

Vilevile, nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Viongozi na Washiriki wote kwa kukubali mwaliko wangu na kuungana nasi katika Mkutano huu muhimu unaobeba Kaulimbiu ya *''Kuchochea Ukuaji wa Uchumi Afrika: Kuongeza Uzalishaji wa Vijana kupitia Mafunzo na Ujuzi'', yaani*

*"Accelerating Africa's Economic Growth: Boosting Youth Productivity by Improving Learning and Skills"*.

***Waheshimiwa Viongozi;***

***Ndugu Washiriki:***

Tunakutana leo kujadili ajenda ambayo ndio moyo wa mataifa yetu – uwekezaji katika rasilimali watu, hususan vijana. Mkutano wetu huu wa leo utaamua ni aina ipi ya uwekezaji unahitajika ili kuleta tija na kuchochea maendeleo ya Bara la Afrika. Hakuna muda mwingine sahihi wa kujadili haya zaidi ya muda huu tulionao leo. Kwa kipindi cha zaidi ya muongo mmoja sasa, Bara la Afrika limepitia ukuaji na uimarikaji mkubwa wa chumi zake katika sekta tofauti. Hali hii ya ukuaji wa uchumi ilifanya bara kuwa na misamiati kama vile; Afrika inakua au Karne ya Afrika (*Africa is rising and Africa's century*).

Misamiati hii ilitokana na vuguvugu la harakati mbalimbali zilizokuwa zikifanyika ili kulikwamua bara hili kutoka kwenye utegemezi wa kiuchumi.

Kulifanyika jitahada za makusudi kuhakikisha bara hili linajenga chumi zake kwa kutumia rasilimali zake ili kuweza kujiletea maendeleo. Kwa baadhi ya nchi na kanda, maendeleo haya yalionekana ila kwa baadhi maendeleo hayakuonekana au yalionekana vipande vipande.

Ni jambo la kusikitisha kuwa, kwa baadhi ya nchi, ukuaji huu wa uchumi haujachangia katika kuhakikisha wanajenga uchumi jumuishi, wala kuchochea uzalishaji wa ajira mpya, hususan kwa vijana. Aidha, mbali na ukuaji huu wa uchumi, bado bara hili limeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile, uhaba wa chakula,

viwango vikubwa vya ukosefu wa ajira, umaskini uliokithiri na ukosefu wa usawa kwenye jamii.

Ni wazi kuwa Bara letu bado linahitaji mageuzi makubwa katika Nyanja zote muhimu za uzalishaji na maendeleo. Na haya ndio malengo na madhumuni ya ajenda ya Maendeleo ya Afrika tunayoitaka ya **mwaka 2063** ambayo imeweka **malengo 7**, nataka nijielekeze kuyazungumzia malengo manne, ambayo ni:-

i. Afrika ambayo mafanikio yake yanajikita kwenye ukuaji jumuishi wa uchumi na maendeleo endelevu;
ii. Bara lenye utangamano kisiasa kwa kuzingatia fikra za kimajumuishi na mwelekeo wa kimapinduzi;
iii. Afrika inayozingatia misingi ya utawala bora, demokrasia, haki za binadamu na utawala wa sheria;

iv. Afrika ambayo maendeleo yake yanatokana na watu kwa kutumia vipaji vyao, hususan wanawake na vijana pamoja na kutoa makuzi bora kwa Watoto.

***Waheshimiwa Viongozi;***
***Ndugu Washiriki:***

Nimeona niyataje malengo haya ili kuona uzito wa dhima na majukumu yaliyo mbele yetu na aina ya uongozi unaohitajika kuhakikisha tunafikia na kutimiza kwa ukamilifu malengo haya. Ni muhimu sisi kama viongozi tuhakikishe kwamba tunaangalia, tutathmini na kusimamia mageuzi yote muhimu ili kuliwezesha bara hili litumie uwezo na rasilimali zake kujikomboa kiuchumi.

Kama nilivyosema awali, Mkutano huu ni sahihi na unafanyika kwa wakati muafaka, hasa ikizingatiwa

kwamba, kwa sasa, Afrika ndilo bara lenye vijana wengi zaidi. Takwimu zinaonesha kuwa  ifikapo mwaka 2050 Afrika itatoa nchi 10 zenye idadi kubwa zaidi ya vijana duniani. Kwa mujibu wa ***World Economic Forum***, zaidi ya **asilimia 60** ya watu Barani Afrika ni vijana walio chini ya **miaka 25**. Aidha, inakadiriwa kuwa, ifikapo **mwaka 2030**, Afrika itakuwa na **asilimia 42** ya vijana wote duniani. Umri wa wastani kwa nchi za Afrika ni chini ya **miaka 20**; hii inamaanisha kuwa bara letu ni bara lenye Watoto na vijana wengi. Kwa tafsiri ya kidemografia, habari hii ni nzuri na vilevile ni mbaya kwetu. Hali hii inaweza tu kuwa nzuri na yenye tija kwetu iwapo tutawekeza kwenye rasilimali watu kwa kuhakikisha uwepo wa afya bora, elimu bora yenye stadi za maisha ili kujenga nguvu kazi yenye tija kama

ilivyo kwa wenzetu wa bara la Asia. Hatma yetu inaweza kuwa mbaya, iwapo hatutofanya uwekezaji sahihi.

Tusipofanya hivi, tutaongeza idadi ya vijana wasio na ujuzi, wasioajirika na vijana wanaokosa mwelekeo wa Maisha hali itakayopelekea vijana hawa kujiingiza kwenye vitendo viovu vya kihalifu na uvunjifu wa amani (Hali hii si ngeni kwa baadhi ya nchi zetu Afrika). Hivyo basi, kwetu sisi tuliopo hapa leo, tujiulize: Je, bara tulilolithiri kwa waasisi ndilo bara tunalotaka wajukuu zetu waje kuliishi? Je, Afrika tunayoijenga leo ni yenye uchumi unaostawi au uchumi unaodumaa?

Majibu ya masuala haya yatatupa mwelekeo wa sera zetu. Ni wazi kuwa viongozi wenye maono hujenga sera zao kwenye maendeleo ya watu na kufuatiwa na

maendeleo ya vitu. Na hapa, mniruhusu ninukuu maneno ya Baba wa Taifa hili la Tanzania. Miaka michache kabla ya kufariki kwake, Mwalimu Julius Nyerere, wakati akihutubia kwenye Mkutano wa Umoja wa Mataifa Jijini *New York* alisema (na hapa nanukuu kwa Lugha ya Kiingereza): ***"Development is people. People are the target, creators and beneficiaries of anything known as development."*** **(**mwisho wa kunukuu). Kwa tafsiri rahisi, "Maendeleo ni watu. Watu ndio walengwa, waanzilishi na wanufaika wa chochote kinachoitwa maendeleo". Kwa mantiki hiyo, hatuwezi kulikomboa Bara letu kiuchumi, kama hatutaelekeza nguvu zetu kwenye maendeleo ya rasilimali watu, kwa kuwapa maarifa na ujuzi unaohitajika katika kuyatumia na kuyabadilisha mazingira yao kwa

manufaa yao. Na huu ndiyo msingi hasa wa maendeleo na mafanikio ya Bara letu.

***Waheshimiwa Viongozi;***
***Ndugu Washiriki:***

Tunapozungumzia uwekezaji katika rasilimali watu, ni kuhakikisha kwamba uwekezaji unaanza tangu mtoto anapozaliwa; kwa maana ya upatikanaji wa lishe bora na chanjo stahiki ili kuondoa udumavu ambao, mara nyingi, hupunguza kiwango cha uelewa na uwezo wa kusoma kwa Watoto. Ili kuhakikisha tunaweka msingi mzuri wa elimu tunapaswa kuwa maandalizi mazuri ya elimu ya awali kwa ajili ya kuwaandaa watoto kimwili, kiakili, kiisimu/kijinsia kiubunifu na kiakili-hisia.

Ili elimu itoe matokeo chanya ni lazima kuwa na mitaala yenye kukidhi matakwa ya soko la ajira. Kwa mfano, uwepo wa Mapinduzi ya nne ya Viwanda kunatulazimisha kwenda na wakati kwa kuhakikisha hatupitwi na teknolojia mpya. Mapinduzi haya ya nne ya Viwanda yameleta mabadiliko makubwa katika sekta zetu za Afya, Elimu, Biashara, Teknolojia pamoja na mahusiano na muingiliano wa kijamii pamoja na usafiri na usafirishaji. Hivyo basi, ni wajibu wetu kuhakikisha Afrika hatuachwi nyuma kwenye mapinduzi haya ya nne kama tulivyoachwa kwenye mapinduzi matatu yaliyopita.

Mwasisi wa Taifa Huru la Afrika Kusini, Hayati Mzee Nelson Mandela, alisema, '***Education is the most Powerful Weapon you can use to Change the world***', akimaanisha kuwa Elimu ndio silaha yenye nguvu zaidi inayoweza

kutumika kuubadilisha ulimwengu. Na hapa nichukue fursa hii kuuelezea umma huu baadhi ya hatua ambazo nchi yetu imechukua ili kukuza na kuendeleza Rasilimali watu.

i. Kutenga fedha kwa ajili ya afua mbalimbali za lishe na huduma za Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto;
ii. Kuanzisha vituo vya elimu ya awali (*Early Childhood Development Centres -ECDCs*);
iii. Mapitio na maboresho ya Sera ya Elimu, mitaala na programu za mafunzo ili ziendane na mazingira pamoja na mahitaji ya sasa ya maendeleo;
iv. Uanzishwaji wa Mfuko wa Kusaidia Kaya Masikini, ujulikanao kama ***Tanzania Social Action Fund (TASAF).*** Lengo la Mfuko huu ni kupunguza umaskini na kuboresha upatikanaji wa huduma za afya na

elimu. Tangu **mwaka 2000**, zaidi ya kaya **milioni moja (01)** zimenufaika na zaidi ya **miradi 731** ya miundombinu ya elimu, afya, maji safi na salama, kilimo na mazingira; njia za usafiri na usafirishaji imetekelezwa.

v. Uanzishwaji wa Programu ya elimu bila malipo kwenye ngazi za elimu ya awali, elimu ya msingi na sekondari kuanzia Kidato cha Kwanza hadi cha sita;

vi. Uwekezaji kwenye elimu ya ufundi na mafunzo ya amali, yaani ***Vocational Education and Training***, ikiwa ni pamoja na kutoa ujuzi bobezi ili kuongeza tija, ushindani na uwezo wa ndani katika kutumia maliasili za nchi yetu;

vii. Kuwezesha vijana kiuchumi kupitia mikopo inayotolewa na Halmashauri kwa Vijana **asilimia 4%,**

Wanawake **asilimia 4%** na Watu wenye Ulemavu **asilimia 2%;**

viii. Kuruhusu Watoto walioachwa masomo hasa wa kike waliopata mimba kuweza kurejea masomoni; na

ix. Kupitia Wizara ya Kilimo Serikali, inatekeleza Programu ya kuwezesha ushiriki wa vijana katika Kilimo Biashara ***(Building a Better Tomorrow Youth Initiative for Agribusiness (BBT-YIA)*** Programu hii inatarajiwa kuongeza ajira kwa vijana kufikia **milioni 3** na kuongeza ukuaji wa sekta ya Kilimo hadi kufikia **asilimia 10** ifikapo **2030 (Ajenda 10/30).**

***Waheshimiwa Viongozi;***

***Ndugu Washiriki;***

***Mabibi na Mabwana:***

Nimezungumzia masuala mengi na kwa kirefu. Sasa, naomba mniruhusu niyataje kwa muhtasari maeneo muhimu yanayoweza kutusaidia kuboresha rasilimali watu ya Afrika, ili yatusaidie kuongoza mijadala yetu:

***KWANZA***, kujidhatiti kutumia rasilimali watu tuliyonayo kwa manufaa demografia yetu, kwa maana ya *"**Reaping the Demographic Dividend":*** Idadi kubwa ya vijana tulionao Afrika ni fursa ya pekee kwa ajili ya mageuzi ya kiuchumi.

***PILI***, Uzazi wa Mpango ***(Managing Fertility Rates)***: Ni lazima tuweke vipaumbele kwenye elimu ya uzazi na mifumo saidizi kwa vijana. Kwa kuwawezesha vijana kufanya maamuzi sahihi kuhusu afya ya uzazi, tunaweza kupunguza tatizo la mimba za mapema, na hivyo kuboresha maisha ya vijana na watoto wanaozaliwa.

*TATU,* **Kuongeza manufaa kutokana na Elimu na Mafunzo tunayotoa nchini kwetu** ***(Improving Learning Outcomes):*** Kwa kuwa elimu ni mwanga na kichocheo cha maendeleo binafsi na ya kijamii, tunahitaji kujikita siyo tu kwenye kuongeza rasilimali fedha kwenye elimu lakini pia kuhakikisha elimu inatoa matokeo yaliyotarajiwa. Na hapa, tunahitaji kuboresha methodolojia za ufundishaji, mitaala na matumizi ya teknolojia katika kutoa elimu.

*NNE,* **Kuongeza Uwekezaji katika Sekta nyingine zinazoleta ufanisi katika huduma za Elimu na Afya** ***(Leveraging Investment in Other Sectors):*** Ni lazima tuwekeze katika miundombinu kama vile Njia za Usafiri, umeme/Nishati, maji na usafi wa mazingira ili utoaji wa huduma za afya na elimu ziwafikie watu wote na ziwe endelevu.

***Waheshimiwa Viongozi;***

***Mabibi na Mabwana:***

***Ndugu Washiriki:***

Kuzifungua fursa katika kuitumia rasilimali watu ya Afrika ni wajibu wa kimaadili na ni sharti muhimu la kiuchumi, kwani kwa kuwekeza katika hifadhi ya jamii, kuongeza rasilimali fedha kwenye elimu na maendeleo ya rasilimali watu, tunaweza kuijenga Afrika yenye mafanikio na jumuishi. Kwa hivyo, inatupasa tuunganishe nguvu za serikali, asasi za kiraia na sekta binafsi ili kufanya uwekezaji unaohitajika na kujenga mazingira wezeshi ya kukua na kuendelea kwa rasilimali hii muhimu, ambayo ni watu wetu. Kwa pamoja, tunaweza kujenga mustakabali mwema wa Afrika, kwa kuhakikisha ndoto za vijana wetu zinatimia.

*Wakati nikihitimisha, nisisitize kwamba suala la maendeleo ya rasilimali watu Afrika, haliwezi kuja kwa kubahatisha na halina mbadala.* Lazima tuwe na mipango Madhubuti ya kuhakikisha rasilimali watu Afrika inaendelezwa kwa manufaa ya bara hili na kwa maendeleo yetu.

Wakati ni sasa; inawezekana; kila mmoja atekeleze jukumu lake kwa nafasi yake tuendeleze bara letu Afrika.

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA…!**

**May God bless our dear Continent, Afrika!**